# PRIMARY END TERM 3 EXAMS
# 2016

# KISWAHIL
## DARASA 4

,
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# KISWAHILI

MUDA: SAA 1 DAKIKA 40

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi zilizoachwa kuanzia 1 - 15.***

Ndege ni viumbe ____1____ kupendeza. Wengine ni ____2____ na wengine ni wakubwa. ____3____ yao huruka ____4____ kwa wale ____5____ hawaruki kama ____6____ kuku, bata na mbuni. Ndege ____7____ mayai ndani ya kiota. Baadaye, ____8____ wadogo huanguliwa. Wao ____9____ makinda.

Kasuku ni ndege ____10____ nyumbani ____11____ hupenda kurudiarudia maneno. Popo ____12____ bundi ni aina ____13____ ndege ____14____ na watu. Popo huruka usiku ____15____ ya mchana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. za | B. vya | C. wa | D. la |
| 2. | A. mdogo | B. kidogo | C. vidogo | D. wadogo |
| 3. | A. Wote | B. Baadhi | C. Zote | D. Kulingana |
| 4. | A. kwa | B. ili | C. na | D. kama |
| 5. | A. ambao | B. ambayo | C. ambaye | D. ambalo |
| 6. | A. vyenye | B. ile | C. tena | D. vile |
| 7. | A. huzaa | B. hutaga | C. huteka | D. hubomoa |
| 8. | A. watoto | B. mtoto | C. vitu | D. mayai |
| 9. | A. inaitwa | B. anaitwa | C. huitwa | D. kinaitwa |
| 10. | A. kinachofugwa | B. anaofugwa | C. analofugwa | D. anayefugwa |
| 11. | A. nasi | B. naye | C. nanyi | D. nazo |
| 12. | A. hadi | B. wa | C. na | D. ya |
| 13. | A. ya | B. za | C. la | D. cha |
| 14. | A. wasiyopendwa | B. isilopendwa | C. zisizopendwa | D. wasiopendwa |
| 15. | A. badala | B. kama | C. hata | D. isipokuwa |

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.***

16. Andika kwa wingi: Tunda hili ni langu.
    A. Tunda hayo ni yetu
    B. Matunda hizi ni zetu
    C. Matunda haya ni yetu
    D. Matunda haya ni langu

17. Kanusha: Enda nyumbani.
    A. Rudi nyumbani
    B. Hutaenda nyumbani
    C. Hujaenda nyumbani
    D. Usiende nyumbani


18. Neno 'kuku' liko katika ngeli gani?
    A. U - I
    B. A - WA
    C. KI - VI
    D. LI - YA

Compiled by Schools Net Kenya. *These e resources are best suited for electronic use only. Not for printing.*
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

19. Jibu la salamu 'shikamoo' ni
A. njema
B. karibu
C. mzuri
D. marahaba

20. Tumia 'amba-' wa usahihi.
Yai ______ limeoza linanuka.
A. ambayo
B. ambao
C. ambacho
D. ambalo

21. Sehemu iliyopakwa rangi ni



A. nusu
B. thuluthi
C. robo
D. humusi

22. Kamilisha: Anakula ugali ______ nyama.
A. kwa
B. na
C. ya
D. ni


23. Tegua kitendawili: Askari mlangoni ______.
A. macho
B. shoka
C. kufuli
D. konokono

24. Kamilisha methali: Mvumilivu hula ______.
A. yote
B. mbichi
C. haraka
D. mbivu

25. Chagua sentensi sahihi.
A. Mtoto msafi anakuja
B. Mbuzi zinakula nyasi
C. Miti ile imekatwa
D. Wageni wote amewasili

26. Kwa wakati uliopita, kitenzi **anacheza** ni
A. atacheza
B. hachezi
C. alicheza
D. hucheza

27. Umbo hili ni



A. mraba
B. mstatili
C. pembe tatu
D. pia

28. Chagua jibu sahihi.
Nyinyi ______ matunda.
A. hauli
B. hawali
C. hamkuli
D. hamli

29. Tumia kiulizi '-pi'. Hiki ni chakula ______.
A. ipi
B. kipi
C. zipi
D. vipi

30. Tarakimu 408 kwa maneno ni
A. mia nne na nne
B. mia nane na nane
C. mia nne na nane
D. mia nane na nne

Compiled by Schools Net Kenya. *These e resources are best suited for electronic use only. Not for printing.*
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

*Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31 - 40.*

Saida aliamka alfajiri na mapema na akafunga safari kwenda kwa mjombake huko Ganze. Pale kituoni aliabiri gari la matatu na wakaondoka salama salimini. Baada ya kusafiri kwa muda wa saa moja, gari lilisimama na baadhi ya watu wakashuka. Wakati hawa watu walipokuwa wakishuka, Saida naye kazi yake ikawa ni kujishughulisha na kuangalia hali ya nchi na watu kupitia dirisha. Hakuangalia mizigo ambayo walioshuka walishuka nayo.

Alipofika mwisho wa safari yake, Saida alishuka na kuulizia mzigo wake. Utingo akapanda juu kuutafuta mfuko wake wa rangi ya nyekundu aliokuwa ameuweka huko darini. Lo! Mfuko haukupatikana. Nguo zake na pesa zote alizokuwa nazo zilikuwa ndani. Alikuwa karibu kuangua kilio lakini alijikaza akasema moyoni, "Bahati mbaya."

Ingawa alipoteza nguo na pesa, alifululiza hadi kwa mjombake. Huko alikaribishwa kwa moyo mkunjufu. Alimwelezea mjombake jinsi alivyopoteza nguo na pesa. Baada ya kusikia hayo yote, mjomba alitoka na Saida moja kwa moja hadi sokoni ili amnunulie Saida nguo zingine. Saida alifurahi sana.

31. Saida aliamka wakati gani?
A. Asubuhi
B. Jioni
C. Alasiri
D. Adhuhuri

32. Mjombake Saida aliishi wapi?
A. Ngozi
B. Ngazi
C. Ganze
D. Kanzi

33. Saida alienda kwa mjomba kwa
A. meli
B. ndege
C. rukwama
D. matatu

34. Wakati gari liliposimama mara ya kwanza, walikuwa wamesafiri kwa muda wa
A. saa moja
B. nusu saa
C. dakika ishirini
D. robo saa

35. Wakati gari liliposimama, watu
A. walipanda
B. walishuka
C. walikula
D. walilala

36. Saida aliposhuka
A. alisahau mzigo wake
B. alipata pesa nyingi
C. aliulizia mzigo wake
D. alilala fofofo

37. Nani alipanda juu ya gari kuutafuta mzigo wa Saida?
A. Dereva
B. Abiria
C. Saida mwenyewe
D. Utingo

38. Mfuko wake Saida ulikuwa wa rangi gani?
A. Nyeusi
B. Nyekundu
C. Nyeupe
D. Manjano

39. Kupotea kwa mfuko ulikuwa karibu kumfanya Saida
A. alie
B. acheke
C. alale
D. akasirike

40. Mjomba alimsaidiaje Saida?
A. Alimpatia pesa nyingi
B. Alimpatia viatu
C. Alimnunulia nguo
D. Alimnunulia gari

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Hapo zamani paliondokea wanyama waliokuwa wakiishi pamoja kama vile kuku, kobe, sungura na chiriku. Katika kijiji hicho, simba ndiye aliyekuwa akikata kesi na kutoa mashauri. Wanyama hao wote waliishi kwa amani na walipendana sana. Hakuna hata mnyama mmoja aliyeishi na binadamu. Wote waliishi pamoja katika kijiji chao naye binadamu aliishi katika kijiji kingine.

Basi siku moja kuku alikuwa na vifaranga na akaenda kuwatafutia chakula. Alipokuwa akitembea aliona kisima naye akataka kunywa maji. Alipofika na kuchungulia, alimwona chatu kisimani. Chatu huyo alisema kuwa alikuwa ametumbukia kisimani siku nyingi zilizopita naye alitaka kuku amsaidie ili atoke. Kuku alikubali na kumsaidia chatu kutoka kisimani.

Baada ya chatu kutoka kisimani alitaka kumla kuku au vifaranga. Kuku naye akamwambia chatu kuwa waende kwa simba ili afanye uamuzi. Walipofika kwa simba, walimwelezea simba kuwa chatu alikuwa akitaka kumla kuku au vifaranga. Simba aliamua kuwa hiyo haingewezekana.

**41.** Mnyama ambaye hajatajwa katika ufahamu ni
A. kobe
B. chiriku
C. twiga
D. sungura

**42.** Mnyama ambaye alikuwa akikata kesi ni
A. simba
B. kobe
C. kuku
D. chatu

**43.** Wanyama hao wote waliishi kwa
A. ugomvi
B. hasira
C. shida
D. amani

**44.** Katika wakati huo, ni wanyama wangapi waliishi na binadamu?
A. Kumi
B. Hakuna
C. Wawili
D. Ishirini

**45.** Vifaranga ni watoto wa
A. chiriku
B. chatu
C. kuku
D. kobe

**46.** Kuku alienda kukata kiu wapi?
A. Kisimani
B. Msituni
C. Sokoni
D. Shuleni

**47.** Kuku alimwona chatu akiwa wapi?
A. Ndani ya nyumba
B. Ndani ya kisima
C. Juu ya mti
D. Kitandani

**48.** Chatu alimtaka kuku amsaidie
A. kuingia kisimani
B. kutafuta chakula
C. kutoka kisimani
D. kujenga nyumba

**49.** Baada ya chatu kutoka kisimani alitaka
A. kumpa kuku zawadi
B. kumla kuku na vifaranga
C. kulala
D. kutoroka

**50.** Nani aliyefanya uamuzi katika kesi ya chatu na kuku?
A. Kobe
B. Chiriku
C. Sungura
D. Simba

Compiled by Schools Net Kenya. *These e resources are best suited for electronic use only. Not for printing.*
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27